



MAKALA YA AFYA/ HEALTH PUBLICATION

UFAHAMU UGONJWA WA KISUKARI (*DIABETES MELLITUS*)

UGONJWA WA KISUKARI NI NINI?

Kisukari ni ugonjwa ambao kiwango cha sukari kwenye damu ni kingi kuliko inavyotakiwa. Hali hii inatokana na mwili kushindwa kusafirisha sukari kwenda kwenye sehemu inayohitajika kama vile kwenye misuli, na hivyo kubaki kwa wingi kwenye damu.

Zipo aina kuu tatu za Kisukari; Kisukari cha aina ya kwanza (*Type 1 Diabetes*), Kisukari cha aina ya pili (*Type 2 Diabetes*) na kisukari cha mimba (*Gestational Diabetes*). Kisukari cha aina ya kwanza hutokea pale ambapo kongosho limepoteza uwezo wa kutengeneza insulinini na hivyo tiba yake ni sindano za insulin. Kisukari cha aina hii huwapata zaidi watoto wadogo. Sababu ya kutokea kwa ugonjwa huu bado haifahimiki vizuri, na aina hii ya kisukari haina tabia ya kurithisha kwenye familia.

DALILI ZA UGONJWA WA KISUKARI

Zifuatazo ni dalili za ugonjwa wa kisukari:

- Kwenda haja ndogo mara kwa mara, hasa wakati wa usiku na
- kunywa maji mengi
- kusikia njaa sana
- kupungua uzito kwa kasi bila sababu
- Kwa watoto wadogo, kukojoa kitandani kwa mtoto ambaye hakuwa na kawaida hiyo

Hata hivyo mtu anaweza kuwa na ugonjwa wa kisukari bila kuwa dalili hizi.

MADHARA YA UGONJWA WA KISUKARI

Baadhi ya madhara ya ugonjwa wa kisukari ni Pamoja na:

- Shambulizi la moyo
- Kiharusi
- Figo kufeli
- Upofu
- Vidonda kwenye miguu
- Kisukari cha mimba husababisha madhara kwa mama na kwa mtoto

WAKATI NIENDE KUONANA NA MADAKTARI WA KISUKARI

- Endapo kuna dalili zozote zilizotajwa hapo juu
- Endapo una vihatarishi kama vile uzito mkubwa, historia ya kisukari kwenye familia, historia ya matatizo ya uzazi kama vile Watoto kufia tumboni
- Endapo umegundulika na ugonjwa wa kisukari utapangiwa siku za kuonana na madaktari wa kisukari mara kwa mara ili kuzuia kupata madhara ya kisukari.

KLINIKI ZA KISUKARI H.M HOSPITAL

- Kia siku za Jumamosi saa tatu hadi saa saba mchana.
- Huduma zinazopatikana ni Pamoja na:
 - Uchunguzi kugundua kama mtu ana ugonjwa wa kisukari
 - Uchunguzi wa kina kwa wagonjwa wenyewe kisukari
 - Elimu ya kuzuia kisukari na elimu kwa wagonjwa wa kisukari
 - Matibabu ya vidonge Pamoja na sindano

Na Daktari bingwa wa magonjwa ya Homoni na Kisukari – HM Hospital-Bunju B

Kwa Huduma ya Kuonana na Daktari Bingwa piga simu namba:

+255 748 053303/+255 754 587900/+255 755 085586